## MKAKATI WA KUHIFADHI MAZINGIRA KATIKA MANISPAA YA SUMBAWANGA

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Uharibifu wa mazingira ya vyanzo kutokana na kilimo cha bustani na mazao ya muda mrefu | Mabonde yote, Kingo za mito, Maeneo tekechu/oevu | a) Kuorodhesha maeneo yote<br>b) Matumizi ya maji yazingatie mahitaji<br>c) Kuweka miundombinu mizuri ya umwagiliaji na ikaguliwe kuhakikisha kuwa maji hayapotei na utaratibu wa matumizi ya maji uzingatiwe<br>d) Kuwaondoa wavamizi wa vyanzo<br>e) Kupanda miti rafiki wa mazingira katika vyanzo vyote | Kudhibiti shughuli za kilimo katika mabonde ndani ya mita 60 hadi mita 200 katika maeneo oevu/tekechu/ chemichemi ambazo ni vyanzo maalumu | MD SUWASA, TFS, Kata,Mtaa /Kijiji | JAN 2017 JUNE, 2018 |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Uharibifu wa vyanzo na Hifadhi unaotokana na uchungaji wa mifugo | Milima/Misitu ya asili Mbizi, Malonje na Millanzi na Misitu ya jamii Malangali, Isofu na Katumba Azimio. | 1. Kubaini maeneo yaliyoharibiwa kutokana na uwepo wa mifugo<br>2. Kuweka utaratibu wa kuwaondoa wafugaji waliovamia maeneo ya vyanzo na Hifadhi kwa kuzingatia sheria zilizopo, misitu, wanyamapori, mazingira na mifugo.<br>3. Kusimamia Sheria Na 20 ya Mazingiraya mwaka 2004 juu ya uharibifu wa Mazingira katika maeneo Maalumu yaliyokatazwa<br>4. Kubaini maeneo yaliyoharibiwa kutokana na uwepo wa mifugo<br>5. Kuweka utaratibu wa kuwaondoa wafugaji waliovamia maeneo ya vyanzo na Hifadhi kwa kuzingatia sheria zilizopo za Misitu, Mazingira na Mifugo. | 1. Kupata idadi ya wafugaji wanaochunga au kufuga katika maeneo hayo.<br>2. Kuwaondoa wafugaji waliovamia maeneo ya vyanzo vya maji, vilima na kuwapeleka maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya malisho | MD, Bonde, SUWASA, TFS, Kata na Kijiji | Jan 2017 – Dec, 2018 |
| | A. Uharibifu wa mazingira unaotokana na uvamizi wa wafugaji katika maeneo ya vyanzo vya maji | Bonde la Lwiche, Vyanzo vya maji vya , Ulinji, Ndua, Malonje, Millanzi, Mzika, Wipanga, | a. Kuainisha maeneo yaliyovamiwa na wafugaji<br>b. Kuainisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji<br>c. Kuwa na takwimu sahihi za uwezo wa malisho kulingana na idadi ya mifugo<br>d. Kushauri wafugaji wa Mwapunguze idadi ya mifugo na wafuge kisasa<br>e. Kusimamia ***Sheria ya Zero*** | 1. Kupata idadi ya wafugaji wanaochunga au kufuga katika maeneo hayo.<br>2. Kuwaondoa wafugaji waliovamia maeneo ya vyanzo vya maji, vilima na kuwapeleka maeneo yaliyopangwa kwa | MD, Bonde, SUWASA, TFS, Kata na Kijiji | January, 2017 DEC, 2020 |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Namabangasa, Muva, Momoka, Senga, Kanantumbi | *Grazing* Mjini<br>f. Kuainisha Stock Routes na kuweka mabango<br>g. Kusimamia Sheria Na 20 ya Mazingiraya mwaka 2004 juu ya uharibifu wa Mazingira katika maeneo Maalumu yaliyokatazwa<br><br>1. Kubainisha mahitaji ya malambo<br>2. Kujenga malambo na visima<br>3. Kutoa eleimu ya matumizi ya malambo na visima kwa wafugaji na wakulima | ajili ya malisho<br><br>Kuujenga na kuendeleza malambo na visima katika maeneo ya wafugaji na wakulima | | |
| 3 | Uharibifu wa vyanzo unaotokana na ukataji miti na uchomaji moto ovyo | Msitu wa Mbizi, Misitu ya Hifadhi ya Jamii ya Malangali, Katumba Azimio na Isofu | 1. Kuhakikisha kuwa kila taasisi , vijiji vinakuwa na eneo la kupanda miti<br>2. Kuandaa vitalu vya miti ifaayo kupandwa katika maeneo yao<br>3. Kuhamasisha jamii ishiriki kudhibiti mioto pindi inapotokea<br>4. Kusaidia vijiji kuandaa Sheria Ndogo ya kudhibiti Moto | Kushawishi vikundi vya kijamii na watu binafsi waanzishe vitalu vya miche miti kwa matumizi mbalimbali ya kibiashara na nishati<br><br>Kuhakikisha kuwa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali na vijiji zinaanzisha mashamba yao ya miti kwa ajili ya matumizi | MD, TFS, Bonde, SUWASA, Kata, Mitaa na Kijiji | January 2017– JUNE 2017 |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1. Kuweka utaratibu utakaodhibiti uanzishaji wa moto<br>2. Kubaini wafanyabiashara wa mazao ya misitu na kuweka utaratibu utakaodhibiti ukataji holela wa miti<br>3. Kufanya doria za mara kwa mara kwa lengo la kubaini wahalifu wa sheria<br>4. Kuwezesha Mitaa na vijiji kuwa na Sheria ndogo ya Kudhibiti Uchomaji Moto | Kudhibiti uchomaji wa misitu na ukataji miti kwa ajili ya nishsti na kuweka utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wake | MD, SUWASA, Kata , Mitaa na Kijiji | January 2017 Decembe 2017<br><br>January 2017 JUNE 2020 |
| | | | a) Kuandaa vitalu vya miche ya miti ifaayo kupandwa katika maeneo ya vyanzo<br>b) Kuhamasisha Mitaa/Vijiji kuanzisha mashamba ya miti<br>c) Kupanda miti katika mipaka ya taasisi<br>d) Kushirikisha jamii juu ya utunzaji wa mazingira | Kuweka mpango mahususi utakaowezesha vijiji kuwa na mashamba ya miti kwa ajili ya matumizi mbalimbali | MD, Bonde, SUWASA, Kata na Kijiji | January 2017 – OCTOBA 2017 |
| | | | Kutoa zawadi kwa watu au vikundi vya watu watakaotoa taarifa za uanzishaji moto na uchomaji moto misitu | Kuchukua hatua kwa viongozi wa eneo husika watakaoshindwa kudhibiti matukio ya moto | MD | JANU. 2017 Endelevu |
| 4 | Kukauka kwa vyanzo kutokana na upandaji wa miti isiyo rafiki na | Vyanzo tegemezi vya maji kama :-<br>1. Ulinji | Kuhakikisha miti isiyofaa kupandwa katika vyanzo inatolewa kwa utaratibu utakaokubalika | Orodha ya watu waliopanda miti isiyofaa na kupiga marufuku upandaji | MD, Kata, Mitaa na | DJanuary 2017 – |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | vyanzo vya maji | 2. Malonje<br>3. Bonde la Mto Lwiche<br>4. Wipanga<br>5. Mlanda na vyanzo vingine | Ufuatiliaji kwa wanaokaidi na kuchukua hatua za kisheria dhidi yao<br><br>Kutoa elimu kwa jamii juu ya upandaji miti inayofaa kuoteshwa katika vyanzo vya maji na maeneo oevu | wa miti yote jamii ya mikaratusi<br><br>Kuwaamuru waikate miti yote isiyo rafiki na vyanzo vya maji mara moja<br><br>Kusimamia Sheria ya Mazingira Na 20 ya Mwaka 2004,<br>Sheria za Maji na Sheria za Bonde.<br><br>Kuweka alama za mipaka katika vyanzo na maeneo oevu au tengefu. | Kijiji | DEC 2020 na Kuendelea |
| | | | Kuhamasisha upandaji miti ya asili katika maeneo ya vyanzo | Kuandaa vitalu vya miti inayofaa kila mwaka<br>Kupanda miti rafiki na mazingira katika vyanzo | MD, Kata, Mitaa na Kijiji | January 2017 DEC 2020 |
| 5 | Uelewa na ushiriki mdogo wa wananchi katika Hifadhi ya Mazingira | Bonde tengefu la Lwiche,<br><br>Vyanzo vyote 25 vya maji ndani ya mipaka ya Manispaa ya Sumbawanga ambayo baadhi | i. Kuandaa Program ya Elimu ya Mazingira<br>ii. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa program ya utoaji wa Elimu ya Mazingira<br>iii. Kuandaa bajeti ya utekelezaji ya kutoa Elimu ya Mazingira kwa Walengwa | Kuanzisha Program ya Elimu ya Mazingira kwa umma<br>Kutoa mafunzo kwa Kamati za Mazingira za Kata, Mitaa na Vijiji | MD, Kata, Mitaa Kijiji | January- 2017 hadi Juni, 2019 |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | yake ni:- Wipanga, Namabangasa, Mzika, Malonje, Ulinji, Muva, Mlanda, Milanzi na vinginevyo.<br><br>Uwanda wa Milima inayozunguka Manispaa ya Sumbawanga | | | | |
| 6 | Mgongano wa matumizi ya ardhi baina ya wadau mbalimbali na uharibifu wa mazingira | Hifadhi ya msitu wa Mbizi, Shamba la EPHATA, Misitu ya Jamii ya Katumba Azimio, Malangali na Isofu | i. Kuandaa mpango unaoonesha Matumizi bora ya Ardhi kwa Manispaa<br>ii. Kusimamia utekelezaji wa program hiyo ya mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi<br>iii. Kuhakiki mipaka ya ardhi,hifadhi za misitu na kushirikiana na Jamii kuweka mipaka. | Kuandaa program ya Hifadhi ya mazingira na mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi | MD, TFS, Kata, Mitaa na Kijiji | January 2017 – DEC 2018 |
| | | | i. Kuhakiki mipaka ya vijiji na Hifadhi<br>ii. Kuwaondoa wavamizi kwa kuzingatia sheria kama wapo<br>iii. Kutekeleza sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 na sheria Namba 7 na 8 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 | Kuhakiki mipaka ya misitu, Mtaa/kijiji na kuifuatilia kwa ukaribu | MD, Kata, Mtaa na Vijiji | January, 2017 – June 2018 |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | iv. Kufanya mapitio ya sheria za kisekta na kuzisimamia ili kurahisisha utekelezaji wake katika kusimamia uharibifu wa mazingira | | | |
| 7 | Uchafuzi wa mazingira unaotokana na utupaji wa taka ngumu na Maji taka katika mito na vyanzo vya maji | Maeneo ya vyanzo, mabonde oevu na maeneo ya wazi au kwenye Makorongo | 1. Kuimarisha mifumo ya majitaka<br>2. Kufanya tathmini ya usafirishaji taka na uteketezaji wa taka<br>3. Kubaini maeneo yaliyoathirika na utupaji wa taka kiholela<br>4. Kuongeza idadi ya maghuba (***Skip Bukets***) za kukusanyia/kuhifadhia taka<br>5. Kusimamia Sheria za Usafi na mazingira<br>6. Kudhibiti matumizi ya mifuko laini ya nailoni inayochafua mazingira<br>7. Kuelimisha jamii juu ya athari za mifuko laini ya nailoni inayochafua mazingira.<br>8. Kuelimisha jamii na kupiga marufuku juu ya ujenzi wa mashimo ya maji taka nje ya eneo la kiwanja cha nyumba au vichochoro na mipenyo baina ya nyumba | Kudhibiti umwagaji na utupaji wa taka ngumu na Maji Taka katika eneo lote la Manispaa<br><br>Kusimamia na kuhakikisha kuwa Taka ngumu zote zimwagwe eneo maalumu lililotengwa kwa kazi hiyo tu huko Mbarika.<br><br>Kusimamia na kuhakikisha kuwa Maji Taka yamwagwe kenywe ***Sewage Oxidation Ponds*** za SUWASA tu. Kusimamia Sheria Na. 1 ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009, Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 na Sheria ya Siku ya Usafi Kitaifa***, "The Environmental Act, (Desingnation of National Cleanliness Day) Guidelines, 2016".***<br><br>Kuga marufuku utiririshaji wa maji taka kutoka kwenye | MD, Kata, Mitaa na Kijiji SUWASA | January 2017– June 2018 |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | makazi, nyumba za biashara, viwandani na kuunganishwa au kuelekezwa kwenye mifereji ya maji ya mvua<br><br>Kukamata watu wanao chafua mazingira na kuwachukulia hatua za kisheria sheria | | |
| 8 | Uchafuzi wa maji unaosababishwa na;-<br>i. Matumizi mabaya ya madawa na mbolea za kilimo<br>ii. Taka na uchafu unaotoka kwenye makazi na hoteli | Mabonde na maeneo ya mito yote, maeneo ya Chemichemi, Bonde la mto Lwiche na sehemu zote zinazotumika kwa kilimo cha bustani na mazao mengine ya chakula au biashara, | i. Kusimamia matumizi sahihi ya madawa na mbolea za kilimo<br>ii. Kuzuia kilimo na shughuli nyingine ndani ya mita 60 kutoka kingo za mito na vyanzo na ***Mita 200 kwenye maeneo ya chemichemi***<br>iii. Kuimarisha mifumo ya maji taka Mjini<br>iv. Kufanya tathmini ya maeneo ya umwagaji maji taka<br>v. Kubaini maeneo yaliyoathirika na utupaji taka holela<br>vi. Kuhakikisha kuwa taka zinazokusanywa zinazolewa na kuondoshwa<br>vii. Kuhakikisha kuwa kila mwananchi anakuwa na chombo cha kuhifadhi taka au mfumo wa kukusanya | 1. Kudhibiti utupaji taka ngumu na Maji Taka.<br>2. Kutambua aina zote za kemikali zinzotumika mashambani na kwenye bustani pamoja na athari zake<br>3. Kuelimisha jamii juu ya athari za kemikali za zinazotumika kwenye kilimo<br>4. Kuchukua hatua za kisheria kwa watu wote wanaotiririsha maji taka kutoka kwenye makazi, viwandani na kuelekeza kwenye mifereji ya maji ya mvua. | SUWASA, Ofisi za Bonde, MD, Jamii | January 2017 JUNE 2018 |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | taka kabla hazijakusanywa na Manispaa<br>viii. Kufanya mapitio ya sheria ndogo za halmashauri zinazosimamia na kudhibiti utupaji taka ovyo<br>ix. Kutoa elimu ya mazingira na afya | | | |
| 9 | Kupungua kwa bioanuai katika Bonde la Mto Lwiche kutokana na kuchoma moto haramu, uwindaji haramu wa ***Swala Maji (Statunga),*** Uendeshaji wa shughuli za kilimo eneo tengefu ***(Environmentaly Sensitive Area***) la Lwiche. | Bonde la Mto Lwiche na Maeneo yenye Chemichemi, | a) Kubaini bioanuai zilizoathirika na<br>b) Kuanzisha na kuimarisha vikundi vya usimamizi wa rasilimali za maji (BMU) na sehemu | 1. Kuorodhesha maeneo tengefu na kushirikisha jamii katika kuyasimamia<br>2. Kudhibiti uharibifu wa bioanuai kutokana na kilimo na uchomaji moto katika maeneo Tengefu | MD, Kata, na Kijiji | Januar y 2017 JUNE 2018 |
| | | | Kusimamia na kuendesha kilimo bora maeneo ya mabondeni | | Ofisi za Bonde, MD, Kata, Mitaa, Kijiji | Januar y 2017–kila Mwaka |
| 10 | Uharibifu wa maeneo oevu/chepechepe | Bonde la Lwiche, | a. Kuanisha maeneo oevu/tekechu yaliyoathirika na shughuli za kibinadamu<br>b. Kuongoa/kunusuru maeneo oevu yaliyoathirika<br>c. Kuanisha na kutenga maeneo tekechu kwa ajili ya kuyahifadhi kisheria<br>d. Kusimamia sheria zilizopo | 1. Kudhibiti shughuli zinaathiri maeneo oevu/chepechepe<br>2. Kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote anayekaidi au kuvunja sheria ya kuharibu maeneo oevu/chepechepe | Ofisi za Bonde, SUWASA MD, Kata, Mitaa na Kijiji | Januar y 2017–Ni Endele vu |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | zinazolinda maeneo tekechu/chepechepe | | | |
| 11 | Kupungua kwa kina cha maji katika mito | Mito yote inayopaswa kutiririsha maji Masika na Kiangazi | 1. Kusimamia matumizi endelevu ya maji<br>2. Kuimarisha ushirikiano wa pamoja kati ya sekta na sekta katika kusimamia sheria na matumizi ya maji<br>3. Kuweka utaratibu utakaowezesha matumizi endelevu ya maji kwa wahitaji | Kusimamia matumizi ya maji katika mito na vyanzo<br><br>Maji yatumike kwa mujibu wa Mahitaji tu iwapo kuna kilimo cha umwagiliaji Kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi bila ya maji kutoka katika vyanzo na mito | SUWASA, Ofisi za Bonde, MD, , Kata, Mitaa na vijiji | January 2017 Endelevu |
| 12 | Uwewpo wa magonjwa ya milipuko kwa jamii maeneo jirani na Manispaa ya Sumbawanga hasa maziwa (ziwa Rukwa na Tanganyika) | Uwepo wa usafiri wa kila siku wa mabasi kutoka Ziwa Rukwa na ziwa Tanganyika | 1. Kuendelea kutoa elimu juu ya madhara ya magonjwa ya mlipuko<br>2. Kuimarisha mifumo ya uzoaji taka na utoaji tiba<br>3. Kuhakikisha usafi na afya za wakazi zinaimarishwa kwa kusimamia usafi wa makazi<br>4. Kutoa taarifa mara moja anapoonekana mtu yeyote anadalili za kuharisha au kutapika au vyote viwili.<br>5. Kuwapeleka mara moja wagonjwa kwenye vituo vya huduma za afya<br>6. Kutoficha wagonjwa au ugonjwa<br>7. Kuchukua hatua za dharura za magonjwa ya milipuko | 1. Kutoa Elimu ya Kupambana na magonjwa ya milipuko kwenye vyombo vya habari, vikao, mikutano, kwa wasafiri wanaotoka na kuelekea ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa kibiashara<br>2. Kufuatilia zote, vijiji wagonjwa wa milipuko mara inapotokea<br>3. Kutoa taarifa kwa jamii juu ya tahadhari za kuchukua<br>4. Kuchukua hatua za | MD, Kata, Mtaa na Kijiji | Jan 2017 – Endelevu |

| NA | TATIZO | ENEO HUSIKA | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | HATUA ZA KUCHUKUA | WAHUSIKA | MUDA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 8. Kuandaa preparedness kits za dawa na response teams | dharura za kudhibiti ugonjwa usienee au kusambaa<br>5. Kuchukua sampuli kwa wagonjwa wanaougua ili kuthibitisha aina ya vimelea vya ugonjwa<br>6. Kutibu wagonjwa wote waliobainika kuwa na magonjwa ya mlipuko | | |
| 13 | Uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele za matangazo, studio za miziki, ngoma za jadi/ vikundi, makelele ya magari | Eneo la Manispaa ya Sumbawanga (maeneo maalumu kama hosipitali, taasisi za umma ka shule, maeneo ya Ibada, | Kuainisha maeneo yote yanayo jihus isha na Machukizo ya Makelele na sauti zilizokithiri na kupata takwimu zao<br>Kutoa matangazo na elimu kwa wanaosababisha kelele | 1. Kupiga marufuku aina zote za kelele zisizostahili<br>2. Kuandaa sheria ndogo na miongozo inayoelekeza viwango vya sauti au kelele zisizofaa mjini na vijijini<br>3. Kuchukua hatua za kisheriakwa watakaokaidi | MD, Kata, Mtaa na Kijiji | JAN., 2017– J na kuendelea |